

# TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

WITO KWA WASANII NA VIKUNDI KUSHIRIKI KATIKA  
TAMASHA LA 38 LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO  
KUANZIA TAREHE 19 HADI 26 OKTOBA 2019

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo inapenda kuwakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kwa ujumla kuomba kushiriki kwa kufanya maonyesho katika Tamasha la 38 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambalo litafanyika katika viwanja vya taasisi (TaSUBa - Bagamoyo) kuanzia tarehe **19** hadi **26 Oktoba 2019**.

Tamasha hili limekuwa na malengo mbalimbali ikiwemo kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wasanii na vikundi vya ndani na nje ya Tanzania kupitia warsha na maonyesho mbalimbali.

Tamasha hili hujumuisha aina mbalimbali za sanaa kama vile **Ngoma, Maigizo, Muziki, Sarakasi, Mazingaombwe, Vichekesho** n.k na maonyesho ya sanaa za ufundi (**Exhibitions**).

TaSUBa inawakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi ili kuweza kushiriki katika tamasha hili kongwe la sanaa na utamaduni wa Mtanzania.

Kauli mbiu ya tamasha la mwaka huu ni ***“Sanaa na Utamaduni Ajira Yangu”***.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia;

Barua pepe: [bagamoyofest@tasuba.ac.tz](mailto:bagamoyofest@tasuba.ac.tz) au [bagamoyofest@gmail.com](mailto:bagamoyofest@gmail.com)

Tovuti: [www.tasuba.ac.tz](http://www.tasuba.ac.tz)

Namba za Simu: +255(0) 655 840 405, +255(0) 787 542 242 au +255(0) 763 408 792